

Maswali

1. Paulo alijuaje pakuenda na ahubiri?
2. Paulo na Sila walienda mji gani?
3. Walikutana na nani na alifanya kazi gani?
4. Alikuwa na imani kwa Mungu?
5. Paulo na Sila walimsaidiaje?
6. Paulo aliponya nani?
7. Nini ilifanyika baadaye?
8. Paulo na Sila walifanya nini gerezani?
9. Unafikiri ni nini ilisababisha tetemeko ya nchi?
10. Mlinzi wa gereza alitaka kujua nini?
11. Paulo na Sila walimwambia mlinzi wa gereza habari ya injili. Nini ikafanyika?
12. Tunaweza kumshukuru Mungu namna gani ?

Majibu

1. Mungu alimuonyesha kwa maono.
2. Filipi.
3. Lidia. Aliuza nguo za zambarau
4. Ndiyo
5. Walimfunza habari ya injili
6. Msichana
7. Mabwana wake walikasirika na wakapeleka Paulo na Sila kwa hakimu. Waliamuru wachapwe na wawatupe gerezani.
8. Waliomba na kuimba nyimbo za kumsifu Mungu
9. Mungu
10. Alichohitajika afanye ili aokolewe.
11. Waliamini, wakaelewa na wakabatizwa.
12. (Weka majibu yako)

SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 1 Mwaka wa 1

50 Mlinzi wa gereza Filipi

Marejeo

Matendo ya Mitume 16:9—34

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu anatulinda na kutuweka salama. Anatusaidia tujue ukweli wake kwa njia nyingi

Maneno maalum

1. Paulo + Sila + ndoto + Filipi
2. Lidia + elewa + batizwa
3. Msichana atabiri + bwana + pata pesa
4. Ponya + kasirika + hakimu
5. Chapa + mlinzi wa gereza + linda + gereza.
6. Ujasiri + nyimbo + tetemeko ya nchi + milango ikafunguka + jiuwe + usijiumize
7. Tisho + salama + amini
8. Nyumba ya mlinzi wa gereza + osha migongo + ubatizo + shukuru



50.1 Paulo alitembea kutoka mji hadi mji akihubiri lakini Mungu alimuonyesha katika ndoto kwamba lazima aende Makedonia. Filipi ni mji ulio Makedonia. Alipokuwa akisafiri alienda na wanafunzi tofauti tofauti. Alienda Filipi na Sila.

50.2 Hapa walikutana na Lidia. Alikuwa akiuza nguo za zambarau Filipi. Alikuwa tayari ni muumini wa Mungu kwa hivyo alisikiliza Paulo na Sila. Alielewa habari ya injili na akataka kubatizwa. Lidia alitaka wakae nyumbani kwake. Jamii yake yote nayo iliamini na wakabatizwa. Ni kwa sababu hii Paulo alitumwa Filipi?

50.3 Walipokuwa wakitembea mjini, waliitwa na msichana fulani akisema, “Watu hawa ni watumishi wa Mungu aliye juu, wanaotunyeshwa njia ya wokovu.” Alikuwa amewaita hivi mara nyingi. Hakuelewa anasema nini. Mabwana wake walipata faida ya fedha kwa kuamini kwamba alikuwa na kipawa cha kutabiri yajayo.

50.4 Paulo aliponya akili yake. Mabwana wake walikasirika sana. Hawakukuwa na mapato tena. Walikasirika sana na wakawapeleka Paulo na Sila kwa hakimu. Wakipaza sauti, “Hawa watu ni wayahudi. Wako wanatufundisha desturi zenye hatuwezi kuamini.” Umati wa watu ulikasirika pia.

50.5 Hakimu walishika Paulo na Sila na kuwatoa mavazi zao. “Wachape,” aliamurisha. Waliwachapa na kuwatupa gerezani. Mlinzi wa gereza aliwachunga. Aliwapeleka chumba cha ndani na kuwafunga kwa mkatale. Hawangeweza kutoroka.



50.6 Paulo na Sila waliomba Mungu awape nguvu na ujasiri. Pia waliimba nyimbo za kumtukua Mungu. Wafungwa wote waliwasikia. Ghafila, kulitokea tetemeko ya nchi. Iitikisa misingi ya gereza. Milango ilifunguka! Vifungo vyote vikatoka kwa wafungwa! Mlinzi wa gereza akaamka - tena milango ilikuwa wazi! Wafungwa wamefunguliwa! Wangetoroka. Ni lazima ataadhibiwa. Akaamua kitu cha kufanya, ni kujiua. Akafuta upanga. Paulo alipaza sauti na kusema, “Usijiumize, sisi sote tungali hapa.”

50.7 Mlinzi wa gereza alileta taa hali anatemeka ili aone Paulo na Sila. Hapo alifahamu kwamba Mungu ndiye aliwaweka salama. Alijua kwamba habari yao hii inatoka kwa Mungu. Akawauliza ni fanya nini ili niokoke?

“Lazima uamini Bwana Yesu Kristo na utaokoka pamoja na jamii yako.”

50.8 Paulo na Sila walipelekwa kwa nyumba ya mlinzi wa gereza. Walimfunza habari ya injili pamoja na jamii yake. Waliamini na kuelewa yote waliyofunzwa na Paulo na Sila. Mlinzi wa gereza na nyumba yake walibatizwa. Mlinzi wa gereza aliwaosha jeraha za migongo halafu wakala chakula pamoja. Wote walifurahi na kushukuru Mungu.